LEARNING BY EAR: Girls EPISODE 4
Sexual Abuse Part 1
Text: Zainab Aziz
Redaktion: Andrea Schmidt/Christine Harjes

Characters:
Anchor…. for Intro/Autro
Bibiy........ main Character
Samera.......girl 15 years old.
Doctor...........male (Adult)
Bamu (Samera"s Uncle)...........Male (Adult)
Mama Samera (Samera"s Mother).......woman (Adult)

Intro:
Ni wakati mwingine tena ninapo kukaribisha kwenye mchezo wa hadithi wa kusisimua katika makala ya Jifunze kwa Kusikiliza. Makala haya maalum yanaangazia maswala yanayowakabili wasichana katika maisha yao ya kila siku. Kisa cha leo ni kuhusu udhalilishaji wa kingono dhidi ya wasichana. Msichana machachari na mwenye busara nyingi Bibiy anamsaidia rafiki yake ambae anakabiliwa na mawazo magumu. Karibu kwenye sehemu ya nne ya Jifunze kwa Kusikiliza.

Sign Tune...........

SCENE 1
(Mama Samera anazungumza na binti yake kwa sauti ya ukali)

MOTHER: Samera kwa nini hutaki kuamka huoni kama unaendekeza uvivu hivyo..eeh husikii. Wewe Samera nakuuliza una shida gani mbona umejibwaga tu hapo kitandani kama vile gunia la viazi? Mimi hata sikuelewi ina maana hujui kuwa saa za kujitayarisha kwenda shule zimetimia? Eeeh! Mtoto wewe siku hizi umebadilka kweli hata sijui unajifikiria wewe ni nani hasa.

SAMERA: (kwa sauti dhaifu) Mama sijisikii vizuri mimi….mimi…Nna..Naumwa siwezi kwenda shule leo mama!.

MOTHER:Hapana Samera sitaki kuongopewa mimi..wewe muongo unaumwa kitu gani hebu inuka hapo sasa hivi au utakiona cha mtema kuni ..si unanijua mie nikikasirika.. haya inuka upesi.

SAMERA: Lakini Mama, Mie naumwa leo sijiwezi (anatapika). Mama wee! Naumwa..naumwa mimi.

MOTHER: Mungu wangu wee mwanangu ana nini..kumbe anaumwa kweli.. masikini mwanangu Oh. Samera, Samera... una nini Samera ..unajisikiaje ee? (Samera anaendelea kutapika).

MOTHER: (Anapiga simu)..Hello, hello Bamu ndugu yangu uko wapi hebu njoo hapa nyumbani nakuhitaji haraka nahitaji msaada wako. Samera mpwa wako mgonjwa kweli ninahitaji kumpeleka hospitali sijui kama unaweza kukodi taxi haraka uje nayo hapa …nyumbani ..Samera Samera (kwa sauti ya wasiwasi) Unajisikiaje sasa mwanangu..Mungu wangu wee kitugani kinaendelea? Samera... Samera!

SAMERA: (Kwa sauti ya udhaifu) Ooh naumwa ... mama wee... Naumwa mimi.
(Sauti ya gari inasikika nje ya nyumba .......halafu linasimama....)

BAMU: (Anagonga mlango na mlango unafunguliwa na kufunga nyuma yake) dada gari iko nje inasubiri. Yuko wapi Samera? Kumetokea nini?..eeh umenambia Samera mgonjwa anaumwa nini?

MOTHER: Bamu ndugu yangu hata sijui nikueleze nini lakini mambo sio mazuri hata kidogo mpwayo Samera anaumwa tena ameshikika ghafla tu..nilikuwa namkaripia juu ya wenda shule mara akaanza kutapika..hebu fanya haraka twende tumpeleke hospitali.

BAMU: Ooh balaa gani tena hii.. kweli Samera anaonekana

taabani sijui ni tatizo gani masikini.. Samera njoo twende hospitali.

SAMERA: (Anavuta pumzi kwa tabu) Mmmmh!.. mmmh!..mama wee..mamaaah.

MOTHER: Basi taratibu mwanangu njoo twende hospitali.
SOUND EFFECTS: (Milango ya gari inasikika ikifunguliwa na kufungwa)

BAMU: Dereva tafadhali endesha gari haraka tuelekee hospitali. (Taxi inaondoka kwa haraka).

MUSIC

SCENE TWO
MOTHER: (Akiwa mwenye wasiwasi mwingi)Daktari, vipi hali ya mwanangu umegundua ana matatizo gani?

DOCTOR: Tulia mama usiwe na wasiwasi. Binti yako yuko kwenye mikono salama..lakini kwanza ningependa kuzungumza nawe..tafadhali bwana naomba utoke nje kidogo.

BAMU: (Akipinga kwa ukali) Kwa nini nitoke nje daktari? Mimi ni mmoja wa familia hii nauliza kwani sina haki ya kujua ni kitu gani kinachomsibu mpwa wangu eeh?

DOCTOR: Samahani itakubidi utoke nje kwani nina haja ya kuzungumza na mama mtoto peke yake kwanza.

BAMU: Daktari labda wewe hunijui mimi bwana mimi ni kaka yake huyu mama Samera unaemuona hapa na kama ningelimuuwa mama yetu basi hata yeye asingeuona ulimwengu hata kufikia kumzaa Samera mwenyewe kwa hiyo sioni sababu ya kunibagua mimi! Wewe tueleze tu daktari samera ana tatizo gani maanake sisi ndio wazazi wake..huyu hapa mama yake na mimi ni mjomba wake.

DOCTOR: Ndugu asante kwa kunifahamisha, nafahamu pia umuhimu wako katika familia hii lakini hata mimi lazima nifuate sheria za kazi yangu kwa hiyo nakuomba kwa heshima utoke nje.

MOTHER: Ni sawa kaka toka tu nje usubiri haina haja ya kuleta ubishi hautatusaidia chochote kaka yangu. Nakuomba umsikilize daktari anavyosema ( Bamu anatoka na mlango unafungwa).

MUSIC......(Muziki wa ala wa masikitiko)

DOCTOR: Mama Samera, hivi mwanao ana umri gani?

MOTHER: ana miaka15, Daktari.

DOCTOR: Tangu lini ameanza kuugua au tangu lini alianza kuonyesha dalili za kuugua?

MOTHER: Kusema kweli daktari mambo haya kwangu yamekuwa ghafla lakini siku hizi kidogo amekuwa na mabadiliko kitabia na kila mara nikimuuliza ana shida gani yeye hunijibu hana neno..hadi hii leo ndipo aliposhindwa kabisa kuinuka kujitayarisha kwenda shule.

DOCTOR: Ahaa sasa... tatizo lenyewe niii... (Muziki wa ala wa masikitiko)

MOTHER: Tafadhali niambie upesi daktari.nataka kujua binti yangu ana nini..mbona unanyamaza..daktari binti yangu ana nini?

DOCTOR: Mama Samera nasikitika kwamba... ukweli wenyewe ni kuwa binti yako ni mja mzito yaani ana mimba!

MOTHER: Eti nini, unasemaje daktari?... hapana haiwezekani!.. eti Samera ana mimba, hapana sio binti yangu ... ooouiiiii! (anaangua kilio) Daktari tafadhali niambie kuwa uchunguzi

wako si sahihi hiyo si kweli kuwa binti yangu Samera ni mja mzito Mungu wangu wee ni mkosi gani huu umeamua kunifika mimi (Analia) Jamani wanawake sisi mbona tunafikwa na mikasa ya kila aina? (Analia) Kwa nini Samera hakuniambia! Je ni nani mwenye mzigo huo.. Oooh! Balaa kubwa imeniingilia nyumbani jamani nitafanya nini mimi? (Analia)

DOCTOR: Tulia Mama Samera nyamaza kulia najua kuwa unasikia uchungu sana.Lakini kwa sasa jambo la muhimu sio kutaka kujua mzigo huo ni wa nani bali la muhimu linalohitajika ni kujua ni hatua gani itakayochukuliwa ili kwanza tuhakikishe Samera amepata afueni. Nyamaza mama tafadhali hebu jikaze kidogo.

MOTHER: (Analia) Oh! Daktari hata sijui wala sisikii neno lolote mimi ninachotaka ni kumjua huyo muovu aliyeniharibia Samera wangu..ooh jamani mwanangu ana umri wa miaka 15 tu tena awe na mimba? Hata siamini! Sitaki kuamini hayo. (Analia)

DOCTOR: Mama Samera, nyamaza kulia. Nafahamu kabisa jinsi unavyo jisikia kwa kweli jambo hililinatia uchungu kwa mzazi yoyote, lakini usijiumize kwa kulia unahitaji nguvu na akili timamu ili kukabiliana na shida hii hebu fikiria hayo kwanza..naam kwa sasa wacha nikamwangalie huyo binti amefikia wapi na matibabu niliyoagiza apewe.
(Daktari na mama Samera wanatoka mlango na unafunguka na kufungika).

BAMU: Ehe dada mama Samera daktari amesemaje? Mbona unalia?..kuna nini?

MOTHER: (Analia) Oooh kaka yangu hata siwezi kuufunua mdomo wangu kukuelezea yaliyotokea.

BAMU: Jikaze dada uniambie..unajua kuwa Samera ni mpwa wangu... yeye ni familia yangu nina haki ya kujua kinachomsibu tafadhali nieleze nami nipate kujua.Je Samera ana tatizo gani?..au Samera amekufa?

MOTHER: Aah tema mate chini samera hajafa..(Analia) Ooh kaka yangu mpwao ametuletea balaa katika familia..hata sijui ni wapi palipoharibika.. Aibu..aibu kubwa ndugu yangu.

BAMU: Lakini mama Samera hujajibu swali langu nakuuliza Samera ana nini?

MOTHER: Oooh... kaka yangu mwanangu mdogo ana…ana (Analia)

BAMU: Samera ana... ana... ndio nini maana yake? Ni aibu gani unayoizungumzia?

MOTHER: Bamu hata sijui kama utaamini nikikwambia.. mpwao ana...ana mimba!

BAMU: haiwezekani! Dada yangu...eti unasemaje? Samera ana mimba ni shetani gani huyo aliyesababisha hayo anastahili adhabu kali zaidi duniani.

MOTHER: Hayo ni kweli kaka yangu hata sijui tutafanya nini..eeh tutafanyaje? Tumekwisha sisi tangu lini mtoto akambeba mtoto mwenzake tumboni? Eeeenh!aibu gani hii Samera ametuletea jamani!

AFRICAN DRUMS

SCENE THREE:
(Samera anazungumza na Bibiy muziki taratibu unasikika kwa mbali)

BIBIY: Samera, pole sana rafiki yangu kwa yote yaliyokufika, lakini nina amini kuwa utafanikiwa kutoka kwenye kipindi hiki kigumu, Samera naomba pia nikupe salamu kutoka kwa wasichana wenzetu wote shuleni wameniambia nikufikishie ujumbe wa kukutakia afueni ya haraka.

SAMERA:Asante (Analia) Bibiy kinachonisikitisha sio matokeo yaliyonifika lakini hasa kinachonisikitisha ni vile makasa huu ulivyo nikuta. Yaani najisikia vibaya sana (Analia).

BIBIY: Una maanisha nini Samera mbona sikuelewi una maana gani unaposema yanayokusikitisha zaidi ni jinsi mkasa huu ulivyo tokea? (Samera analia) Tafadhali rafiki yangu mzuri nyamaza kulia hebu kusanya mawazo yako pamoja..tulia Samera nieleze ili sote wawili tushirikiane kutafuta suluhisho.

SAMERA: Bibiy hebu niambie ungefanyaje iwapo ingetokea kuwa unabeba uja uzito wa mtu kutoka kwenye familia yenu?

BIBIY: Eti nini una maana gani Samera?

SAMERA: Ndio Bibiy. Nina maanisha kuwa mimba hii mimi ni ya mjomba wangu Bamu! (Analia)

BIBIY: Loo!.. Samera una hakika rafiki yangu kuwa haya unayoniambia ni ya kweli? Hebu endelea niambie kila kitu bila kunificha. Ooh pole sana rafiki yangu.

SAMERA: Mmmh... mmmmh... ni vigumu sana mtu kuweza kuamini...

BIBIY: Mimi nitaamini yale yote utakayoniambia Samera liwalo na liwe na wala sitakulazimisha kwa nguvu uniambie iwapo hutaki kuzungumza zaidi rafiki yangu..lakini nakuhahikikishia kuwa wewe hupaswi kulaumiwa kwa yale yaliyokukuta.

SAMERA: (Analia) Uncle Bamu alikuwa mtu mkarimu sana kwangu..mara nyingi alikuwa akiniletea zawadi mbalimbali na wakati mwingine alikuwa ananichukua kwenye matembezi mwishoni mwa wiki hivyo basi tukawa marafiki sana na mjomba wangu nilimpenda na kumuheshimu. Lakani wakati fulani mwaka jana Uncle Bamu akaanza kunipeleka nyumbani kwake

mara kwa mara na tukifika huko ananiambia niangalie zile picha chafu chafu.

BIBIY: Yaani mjomba wako akakushawishi kuanza kuangalia magazeti yenye picha chafu pamoja na kaseti za video?

SAMERA: Ndio! Alikuwa akiniambia kuwa hiyo si tabia mbaya eti mimi ni msichana mkubwa na ninaruhusiwa kuangalia picha hizo (analia). Saa nyingine uncle Bamu alikuwa ananishika maziwa yangu na kunipiga hata visi wakati mwingine..Bibiy hayo yaliendelea kwa muda na baadae mambo mengine yakafuatia..kwa kweli sikupendezwa na mambo hayo lakini Uncle Bamu alianza kunitisha na kunionya kuwa nisimwambie mtu yoyote basi na mimi nilifikiri pia labda nikisema hakuna mtu atakae niamini ndio maana hata mama yangu sikumwambia (Analia).

BIBIY: Pole sana rafiki yangu Samera – Lo huu ni udhalilishaji kingono dhidi ya watoto wa kike..wajua Samera wahanga wa ukatili huu mara nyingi huwa wanaamini kuwa wao ndio wanapaswa kulaumiwa kwa kilichotokea najua hata wewe unakufikiria kuwa unastahili kulaumiwa lakini Samera ondoa shaka hiyo moyoni mwako kwani itachangia kukudhuru afya yako badala ya kukusaidia.

SAMERA: Bibiy unadhani mama yangu ataniamini nikimweleza haya? Kwa sababu licha ya mjomba wangu kunitisha nilijaribu wakati Fulani kutaka kumueleza kuwa mimi simpendi uncle Bamu, wee karibu aninyonge..basi nikaingiwa na uoga kabisa kuzungumza chochote juu mjomba wangu huyo..sasa mambo yameniharibikia kabisa hata sijui nifanyeje (Analia).

BIBIY: Lo masikini rafiki yangu pole sana kwa mkasa uliokufika. Huyu mjomba wako hata sio binadamu yeye ni mnyama mbaya sana. Mimi nafikiria kama kuna mtu angepaswa kukulinda zaidi ni yeye na wala sio vinginevyo. Kwa sababu anajua kuwa wewe ni mtoto na hivyo hapaswi kukuhusisha katika tendo la ndoa. Tendo la ndoa dhidi ya mtoto ni kinyume cha sheria loo huyu

mzee anahitaji kutupwa korokoroni maisha yake yote.. lakini usijali rafiki yangu yote haya yatakwisha.

SAMERA: (Analia) Oooh... sidhani kama yatakwisha. Nimechanganyikiwa hata silijui la kufanya Bibiy. Mambo hayatakuwa sawa tena maishani mwangu kuna tofauti kubwa mimi ni mja mzito sasa...sijui maisha yangu yatakuwaje! (Analia) Naogopa sana.

BIBIY: Samera, Samera tafadhali hebu nisikilize...najua kuwa umo katika lindi la majonzi lakini nataka ujue kwamba wewe huna makosa yoyote na wala hupaswi kulaumiwa hilo narudia ena kukwambia, hata nyanya yangu ameshawahi kunieleza kuwa baadhi ya ndugu katika familia wanaweza kuwa na tabia za ajabu ajabu, nyanya aliniambia kuwa udhalilishaji wa kimapenzi unasababisha athari kubwa ya kimawazo na kumwacha muhanga akiiishi maisha yasiyokuwa na raha hata kidogo..lakini wewe rafiki yangu umefanya jambo la muhimu sana kwani umeweza kuzungumza tatizo linalokukabili.

SAMERA: Bibiy unafikiria huyu mjomba wangu tutamfanyaje mimi nataka nimkabili nimwambie kuwa simpendi hata kidogo yaani namchukia kabisa (Analia).

BIBIY: Samera, sikiliza eeh. Kwa sasa hatutamkabili mjomba wako kwani lengo letu kwanza ni kuhakikisha kuwa wewe mwenyewe umepata afueni halafu baadae ndio tutajua la kufanya..Samera wacha niondoke kwa sasa ili nijaribu kuwatafuta wahusika watakao kusaidia ..huyu mjomba wako lazima afikishwe mbele ya sheria.

SAMERA: sawa Bibiy nakusikiliza lakini kama ni amri yangu ningetaka huyu mjomba wangu ahamishwe kabisa karibu na wasichana wengine ili wasije wakafikwa na mashaka yaliyonifika mie.

BIBIY: ndio maana rafiki yangu nakwambia niache niondoke maanake lazima huyo mjomba wako akione cha mtema kuni

kilicho mtoa kanga manyoya…pumzika Samera nitarudi kukutembelea wakati mwingine.

SAMERA: Kwaheri Bibiy asante sana kwa ushauri wako.

MUSIC

Autro: hakika kuwadhalilisha wasichana kimapenzi ni hatia, Samera nae amenasa kwenye mtego. Je Bibiy atafanyaje kumuokoa rafiki yake huyu. Usikose kuisikiliza sehemu ya pili ya kisa hiki cha kusisimua wiki ijayo katika mfululizo wa makala haya ya Jifunze kwa Kusikiliza. Naam iwapo ungependa kuusikiliza tena mchezo huu au ungetaka pia kumjulisha rafiki ili nae ausikilize basi tembelea tovuti yetu katika anuani ifutayo HYPERLINK "http://www.dw-world.de/lbe" www.dw-world.de/lbe. Tukutane tena wiki ijayo ili tujue ni kipi kitakacho mfika Bamu, mjomba wake Samera? Hadi wiki ijayo panapo majaliwa yake Mola kutoka Jifunze kwa Kusikiliza kwaheri.

END